


Zama ni mkubwa!

 Michael Oguttu

 Vusi Malindi

 Matteo E. Mwita

 2

 Kiswahili SW



Mdogo wangu anachelewa kuamka. Mimi naamka mapema kwa sababu mimi ni mkubwa!



Mimi ndiye ninayeruhusu jua kuingia ndani.



“Wewe ni nyota wangu wa asubuhi,” anasema mama.



Naoga mwenyewe, sihitaji msaada.



Naweza kustahimili maji ya baridi na sabuni ya bluu inayonukia.



Mama ananikumbusha, “Uisahau kupiga mswaki.” Namjibu, “Kamwe, sio mimi!”



Baada ya kuoga, nawasalimu babu na shangazi, na kuwatakia siku njema.



Najivisha nguo mwenyewe. "Mimi ni mkubwa sasa mama," ninamwambia.



Ninaweza kufunga vishikizo na kurekebisha viatu vyangu.



Na ninahakikisha mdogo wangu anapata taarifa zote za shule.



Darasani najitahidi sana katika kila kitu.



Ninafanya hivi vitu vyote vizuri kila siku. Ila kitu ninachokipenda sana ni kucheza na kucheza.



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Zama ni mkubwa!

 Michael Oguttu

 Vusi Malindi

 Matteo E. Mwita

